

# **TARATIBU ZA KUZINGATIA KATIKA KUTHIBITISHA WALIMU KAZINI KATIKA UTUMISHI WA UALIMU.**

*Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.*

## **1.0. Utangulizi.**

Makala hii inakusudia kuelezea taratibu zinazopaswa kuzingatiwa na Idara ya Utumishi wa Walimu wakati wa kuthibitisha walimu kazini na wajibu ambao mwalimu anapaswa kuutekeleza wakati wa kipindi cha majaribio. Kabla ya kuelezea taratibu na wajibu tutaangalia zana ya kuthibitishwa kazini na nani aliyepewa mamlaka ya kuthibitisha walimu kazini katika Utumishi wa Ualimu.

## **2.0. Kuthibitishwa Kazini.**

Ajira ya mwalimu haikamiliki hadi awe amethibitishwa kazini. Mara mwalimu anapojiriwa hujaza mkataba na mwajiri wake na kwenye mkataba ameelezwa wazi kuwa atakuwa katika kipindi cha majaribio (probation period) kisichozidi miezi 12. Madhumuni ya kipindi cha majaribio ni kutoa nafasi ya kutathmini uwezo wa mwalimu wa kufanya kazi na kama anastahili kuajiriwa katika utumishi wa umma. Mwisho wa kipindi cha majaribio, mwalimu atapewa barua ya kuthibitishwa kazini iwapo atamudu majukumu yake vizuri.

## **3.0. Je, Mwalimu Huthibitishwa Kazini Na Nani?**

Wajiri wa Walimu ni wengi na mamlaka yao ya ajira na nidhamu ni Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD). Walimu utofautiana na makundi mengine ya watumishi wa umma ambapo mwajiri na mamlaka ya ajira ni huyo huyo. TSD ndiyo humthibitisha kazini mwalimu. Hii ni kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya 2002 kifungu 6(4) na Kanuni Na. 6(h) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003.

### **3.1. Utaratibu Wa Kuzingatia Katika Kuthibitisha Walimu Kazini.**

Baada ya kuangalia kuthibitishwa kazini ni nini na yule aliyepewa dhamana ya kuthibitisha walimu kazini, tuangalie taratibu ambazo Idara ya Utumishi wa Ualimu inapaswa kuzingatia wakati wa kuthibitishwa walimu. Ili mwalimu aweze kuthibitishwa kazini zipo hatua kadhaa za kufuata. Hatua ya kwanza ni msimamizi au mwajiri wa mwalimu kutoa taarifa ya utendaji kazi wa mwalimu kwa mamlaka ya ajira (TSD) miezi mitatu kabla ya kipindi cha majaribio kuisha. Katibu TSD Wilaya atawasilisha mapendekezo ya walimu kuthibitishwa kazini kwa kamati ya wilaya ambayo nayo hutoa maoni yake kwa kamati ya Mkoa (TSD). Kamati ya Mkoa hutoa maamuzi na Katibu TSD Mkoa huwaandikia barua za kuthibitishwa kazini walimu wote waliokubaliwa.

Mwalimu hataweza kuthibitishwa kazini iwapo atashindwa kudhihirisha kuwa anamudu majukumu ya ajira yake katika muda wa majaribio. Mwalimu anaweza kuongezewa muda wa kipindi cha majaribio mara moja tu kwa muda usiozidi nusu ya kipindi cha majaribio cha mwanzo mradi tu kuwe na matumaini ya kuboresha utendaji. Iwapo mwalimu atashindwa kudhihirisha kumudu majukumu yake ataondolewa kazini.

3.2. Wajibu wa Mwalimu katika kuthibitishwa kazini.

Ili mwalimu aweze kuthibitishwa kazini anapaswa kumudu vizuri majukumu yake aliyopewa mara baada ya kupewa barua ya kuteuliwa katika nafasi aliyoiomba. Baada ya kuhitimisha kipindi cha majaribio mwalimu hupewa barua ya kuthibitishwa kazini.

**4.0. Hitimisho.**

Kuthibitishwa kazini ni jambo la msingi katika mchakato wa ajira ya mwalimu. Ili kazi hii iweze kuwa na mafanikio na kumaliza malalamiko ya kutothibitishwa kazini kwa muda mrefu kwa walimu, walimu wote katika utumishi wa walimu wanapaswa kushirikiana na Idara ya Utumishi wa Ualimu katika jukumu la kuthibitisha walimu kazini.

Iwapo una maoni au maswali tafadhali tuandikie:

Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Tume ya Utumishi wa Umma,  
S.L.P. 9143  
**DAR ES SALAAM.**